MTAZAMO WA KIISLAMU KUHUSU KAMPENI ZA UCHAGUZI MKUU

Na

Abdulla Talib Abdulla

UTANGULIZI

Sifa njema zote anastahiki Mwenyezi Mungu ambae humpa utawala amtakae na kumuondoshea ufalme amtakae; Sala na salaam zimshukie Mjumbe wake Muhammad SAW na wafuasi wake wote hadi Mwenyezi Mungu atakaporithi ardhi na vilivyomo. Ama baada ya hayo:-

Wakati tunakaribia katika uchaguzi mkuu wa Zanzibar unaotarajiwa kufanyika Oktoba 31 mwaka huu, tayari nyoyo za baadhi ya watu zimeshaanza kupigapiga kwa khofu na waja wema wamekuwa wananyanyua mikono yao mbinguni kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kuupitisha uchaguzi huo kwa salama na amani; na Zanzibar yetu idumu katika Amani. Dua hizi za waumini zimekuwa zikifanyika kwa makundi, vikundi vidogo na watu mmoja mmoja, kwa dhahiri na kwa siri.

Kwa nini wengine bado wawe na khofu pamoja na kuwepo dhamira ya kisiasa ya maridhiano?! Kwa kweli watu hawa hawalaumiki kwa vile wameangalia yaliyopita nyuma kwa kufuata kauli ya Allah Mtukufu ***((Basi zingatieni enyi wenye akili))*** Al-Hashir : 2; na hadithi ya Mtume S. A. W: isemayo: ***((Hadungwi Muumini katika tundu moja mara mbili)).*** Kwa wachamungu hawakuona njia bora zaidi ila kumuelekea **Yule ambae atakalo tu ndio huwa** kwani amesema na kauli yake ni haki ***((Na wanapokuuliza waja wangu hakika Yangu mimi Basi mimi nipo karibu naitikia maombi ya mja anaponiomba)) Al Baqara:186.***

MAZINGATIO KWA WAGOMBEA NA WASIMAMIZI WAKATI WA KAMPENI

Mwenyezi Mungu ametuteremshia Mitume na vitabu ili vituongoze na akajaalia utekelezekaji wa dini na mwenendo wa maisha utegemea juhudi za mwanadamu mwenyewe kwa nyenzo alizopewa na Muumba wake. Na kwa msingi huo tunaona Mitume wote wakiwemo Mitume wakuu (*ulul azmi*) Muhammad SAW, Issa Alayhi Salaam, Mussa AS, Ibrahim AS na Nuhu AS namna walivyochukua juhudi kubwa isiyo na kifani ili kuhakikisha kuwa nyumati zao zinakuwa kwenye salama na amani ya dunia na akhera. Allah amemsifu Mtume Muhammad SAW aliposema ***((Amekufikieni mjumbe alie jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha (sana) yale yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni (kukutakieni kheri) na kwa waumini ni mpole na mwenye rehema))*** Tauba: 128. Na akamsifu tena kwa kusema ***((Huenda ukaingamiza nafasi yako kwa***

kutokuamini kwao)) Shuaraa: 3. Na akamsifu Nabii Nuhu aliposema ***((Hakika mimi nimewalingania watu wangu usiku na mchana … kisha nikawaita kwa jahari, kisha nikawatangazia kwa kelele tena nikasema nao kwa siri))*** Nuhu: 5 – 10.

Juhudi hizi zote walizichukuwa kwa sababu walijuwa kwa yakini kuwa ***((Hakika Allah hayabadilisha yaliyo kwa waja mpaka wayabadilishe yaliyo nyoyoni mwao))*** Raad: 11. Hivyo kukaa na kuomba dua tu hakutotosha kama nyoyoni mwetu hatujambadilisha. Maneno na matendo yetu ni lazima yaende sambamba, bali ni wajibu pia kuwaqlingania na wengine ili waidumishe imani iliyopo. Amesema Sayyidina Omar. ***"Asikae mmoja wenu akawa hatafuti riziki huku anasema Mola wangu niruzuku. Mola wangu niruzuku hali anajua kuwa mbingu hazinyeshi dhahabu wala fedha))***. Hivyo kuomba dua tu kuwa tujaaliwe kuwa na amani na utulivu hakutoshi huku tunajua kuwa Allah hateremshi askari wa kuzuwia ghasia kutoka mbinguni. Hivyo, tunatakiwa tuchukue juhudi kwanza na hapo ndio msaada wa Mwenyezi Mungu utakapokuja, kama alivyosema ***((Na wale waliochukua juhudi kwa ajili yetu bila ya shaka tutawaongoza katika njia zetu. Na hakika Allah yuko pamoja na watendao wema))*** Ankabuti aya ya 69. Kudumisha amani na utulivu ni katika kufanya juhudi kwa ajili ya Allah kwani Yeye SW ndie aliesema ***((Lau kama si Allah kuwazuilia watu baina yao juu ya wengine basi ingefisidika ardhi))*** Al-Baqara: 251.

Alhamdulillah, wanasiasa wametiliana saini katika maadili ya uchaguzi. Wamechukua ahadi mbele ya Allah Subhanahu wataala, kati yao na mbele ya wazanzibari kuwa watafanya kampeni za kistaarabu. Wamekubaliana kuwa wasifanye fujo, wasichokozane, walinde amani, wadumishe utulivu, wavumiliane nk,. Hakika maneno yanayotoka moyoni hutua moyoni na yanayotoka mdomoni huwa hayakiuki masikio. Tuwe na yakini **ahadi hii tuliyoichukua haitoishia hapa duniani** bali kila Mja ataulizwa na Mola wake namna alivyoitimiza. Tujue kuwa Allah hutuangalia nyoyoni kama alivyosema katika aya tuliyotangulia kuitaja na huleta mabadiliko kwa mujibu wa nyoyo zilivyo.

Ni lazima kila mmoja kwa nafasi yake na uwezo wake achukue juhudi ili kuiepusha jamii na balaa na kudumisha uadilifu kwetu na kwa vyombo vyenye dhima katika uchaguzi. Iwapo tutakuwa wakweli na Allah anatushuhudia na malaika wanaandika tunayoyasema bila shaka tutakuwa kama inavyosema Qur-ani ***((Iwapo watataka kutengeneza basi Allah atawawafikisha))*** Nisai: 35. Aidha huenda tukawa katika wale aliowasifu Mtume S. A. W aliposema

”Viongozi wenu wema ni wale mnaowapenda nao wakakupendeni, mnaowaombea dua nao wakakuombeeni….” Muslim.

Ahadi nyingi hutolewa na wagombea wakati wa kampeni. Bila shaka ahadi hizi nazo haziishii katika upepo bali ni zenye kuandikwa na kuulizwa mbele ya Allah. Mwenyezi Mungu anatujuwa kama tuna dhamira ya kweli ya kutekeleza ahadi hizo au kama tunadanganya ili tupate muradi wetu huku tukijisifu kuwa tumeshabobea kisiasa kwa kufanya utapeli wa maneno. Mwenyezi Mungu anasema **((Na tekelezeni ahadi (mnazozitoa); hakika ya ahadi ni yenye kuulizwa))** Israa:34. Pia Mtume SAW amesema **”Alama za mnafiki ni tatu, akizungumza husema uongo, akiahidi hukhalifu miadi na akiaminiwa hufanya khiana”.** Hivyo tujihukumie wenyewe vipi tunataka kukutana na mola wetu katika maisha ya milele. Maisha ya dunia na uzuri wake hayana thamani mbele ya yale ya milele. Tutambue kuwa niwengi wamepita katika nafasi tunazozigombania lakini hivi sasa wameshatanguli mbele ya haki.

Niaminivyo ni kuwa kila kiongozi mwenye dhamana na mchunga ambae nyuma yetu kuna kundi kubwa la watu wanaomfuata na kusikiliza atafikiria wakati Allah akituuliza ***((Jee ndio yanayotarajiwa kwenu iwapo mtapata ukubwa (mamlaka/dhamana) mfisidi katika ardhi (kwa kutofanya uadilifu) na kuwakata (kuwabagua) jamaa zenu)).*** Muhammad:22. Kwa maana hiyo atakuwa hadhir kuutekeleza mkataba na dhamana aliyoibeba ili kuinusuru jamii yetu isije ikaingia katika janga ambalo litawasibu wote kama alivyosema Allah (S. W) ***((Na jiepushe na balaa ambalo halitowapata wale waliodhulumu nafsi zao miongoni mwenu pekee (bali liwapata wote). Na tambueni kuwa hakika Allah ni mkali wa kuadhibu)).*** Al-Anfal: 25

Tutangulizeni maslahi ya wengi kuliko maslahi binafsi na tumpige vita shetani ambae ni adui yetu mkubwa. ***Tutambue kuwa upinzani sio uadui na utawala sio ubabe****,* hivyo yeyote atakaeshinda ni mmoja miongoni mwetu na ana haki, na hilo tayari ameshaandikiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu tokea hajazaliwa. Tujitahidi katika kampeni lakini tujuwe kuwa ***juhudi zetu hazitobadilisha kadari***. Amesema Mtume SAW ***”Lau kama umma utakusanyika ili wakunufaishe kwa jambo hawatokunufaisha ila kwa jambo ambalo ameshakuandikia Allah... Zimeshasimama kalamu na wino umeshakauka***”. Pia alieshindwa ni lazima apewe heshima yake anayostahiki wala asibughudhiwe, asinyanyapaliwe au kuchezwa shere.

Kwa mnasaba huu ni wajibu wetu pia kuvihifadhi na kuviheshimu vitu vyote vinavyostahiki kuheshimiwa na kuhifadhiwa.

- Kuhifadhi dini na misingi yake isivunjwe.
- Kuhifadhi nafsi na damu za watu zisimwagwe wala kunyanyaswa.
- Kuhifadhi mali za watu zisiharibiwe.
- Kuhifadhi heshima za watu zisivunjwe.
- Kuhifadhi akili zisigubikwe, zisipotezwe wala kuharibiwa

Pia inapasa tukumbuke kuwa maadili yasiishie baina ya wanasiasa tu; bali makundi mengine pia yana maadili yao yanayopaswa kuheshimiwa kama inavyotakwa yaheshimiwe mabango ya kisiasa. Tunapopita nyumba za ibada tuzipe haki yake, tusifanye mikutano au kuweka malaudi spika katika nyakati na sehemu ambazo zitawaharibia watu sala zao. ***Allah , Allah na Quran. Ni maneno ya Mwenyezi Mungu Matukufu***. Yatumike kwa lengo lililokusudiwa na sehemu iliyokusudiwa. Tunaweza kutaka baraka za Qurani katika mambo yetu kumbe Qurani ikawa inatulaani!? Hivyo ni kweli tunaiheshimu Qurani iwapo kwenye jukwaa wanashuka wacheza ngoma walio nusu uchi halafu anapanda msoma Qurani?! Au Qurani inasomwa huku ngoma zinapashwa moto au waimba kwaya na stage show wanajifunga vibwebwe ili akishuke wapande wao?! Hii si kukifanyia mchezo kitabu cha Mwenyezi Mungu? Mcheni Mwenyezi Mungu enyi wasomaji mliopewa sauti nzuri kama ya nabii Daud na mkumbukeni Allah anaposema***: ((Sema kwa Mwenyezi Mungu, na aya zake na Mtume wake ndio mnafanya istihzai? Msitoe udhuru kwani mumeshakufuru baada ya imani yenu...))*** Tawba :65-66.

MAZINGATIO KWA WAPIGA KURA

Natambua kuwa kuna mitizamo tofauti ya waislamu kuhusiana na suala zima la kushiriki katika chaguzi na kampeni. Ingawa binafsi yangu sipendelei kuhudhuria mikusanyiko ya kampeni kwa mazingira yanayokuwepo lakini hufuatilia kwa karibu ili nielewe yaliyozungumzwa na kuyapima vyema. Ninaheshimu rai za watu kama ambavyo kinachonithibitikia kuwa ndio sahihi hukishika kwa meno ya gego. Kwa mantiki hiyo ninaamini kuwa ***"kisichowezekana chote hakiwachwi chote"*** na kuifananisha jamii ya kizanzibari na Makafiri wa Kikureishi nahisi ni *"Kiasi maal faarik"* yaani kujengea hoja hukmu au mfano usiofanana.

Rais wa Zanzibar ndie anaekuwa waliyul amri, ndoa za mabinti wasiokuwa na Mawalii zitaozeshwa kwa niaba yake na utekelezwaji mambo mengi utategemea ridhaa yake. Aidha, viongozi mbali mbali wa kidini na kijamii watateuliwa na yeye na utoaji vipaumbele na utumiaji wa rasilimali kwa kiasi kikubwa utategemea sifa zake na uadilifu wake. Hivi nisisikilize sera zao na kupima ili kujitahidi kwa uwezo wangu kuchagua atakaekuwa na maslahi zaidi kwa dini yangu na dunia yangu?!

Wabunge, wawakilishi na madiwani ndio watakaoniwakilisha na kunisemea katika mabaraza yanayofunga na kufungua mambo *"Majaalis ahlil hil-li walaqdi".* Niache wengine wanichagulie au nijitahidi kumchagua ninaedhani kuwa ni mwenye sifa na uwezo wa kuniwakilisha vyema kwa kutetea rai zilizo sadidi na kuniletea maendeleo.

Ninayakini kuwa Allah hatoniuliza kuhusiana na majukumu aliyoyafanya kiongozi bali ataniuliza majukumu na dhamana zangu. Kama ambavyo naamini kuwa nitaulizwa juu ya neema zote nilizoneemeshwa kwazo ikiwemo elimu na nafasi ya kuchagua watakaowaongoza au kuwatawala watu. Kwa msingi huo sina budi kujitahidi ili wapatikane viongozi walio wema, wanaofanya mema nakulingania mema.

Ili tuwe makini kwa kufuatilia kwa karibu na umakini harakati zote nitakupelekeni katika suratu Naml ili tuangalie tafsiri na mafunzo tunayoyapata asaa tukafahamu na kutoa maamuzi yaliyo mzuri zaidi katika usikilizaji wetu na utoaji maamuzi. Allah anasema katika suratun Naml aya ya 15 hadi 42:-

((15. Na hakika tuliwapa Daudi na Sulaiman elimu, na wakasema: sifa njema zote ni kwa Mwenyezi Mungu aliye tufadhilisha kuliko wengi katika waja wake Waumini. 16. Na Sulaiman alimrithi Daudi, na akasema: Enyi watu! Tumefunzwa lugha za ndege, na tumepewa kila kitu. Hakika hii ni fadhila iliyo dhaahiri. 17. Na alikusanyiwa Sulaiman majeshi yake ya majini, na watu, na ndege; nayo yakapangwa kwa nidhamu. 18. Mpaka walipofika kwenye bonde la wadudu chungu, alisema mdudu chungu mmoja: Enyi wadudu chungu! Ingieni majumbani mwenu, asije kukupondeni Suleiman na majeshi yake bila ya wao kutambua.19. Basi (Suleiman) akatabasamu huku anacheka kwa neno lake, na akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Nizindue niishukuru neema yako uliyonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kutenda mema uyapendayo, na uniingize kwa rehema yako katika waja wako wema. 20. Na akawakagua ndege, na akasema: Imekuwaje, mbona simwoni Hud-hud, au amekuwa miongoni mwa walio ghibu? 21. Kwa yakini nitamuadhibu kwa adhabu kali, au nitamchinja, au aniletee hoja ya kutosha. 22. Basi (Hud-hud) akakaa si muda mrefu (akarejea) na akasema: Nimegundua usiloligundua wewe, na nimekujia hivi kutoka nchi ya Sabai, na nakuletea khabari za yakini. 23. Hakika mimi nimemkuta mwanamke anawatawala (watu wa huko), naye amepewa kila kitu, na anacho kiti cha enzi kikubwa. 24. Nimemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Mwenyezi Mungu; na Shet'ani amewapambia vitendo vyao na

akawazuilia Njia. Kwa hivyo hawakuongoka, 25.Na hawamsujudii Mwenyezi Mungu ambaye huyatoa yaliyo fichikana katika mbingu na ardhi, na anayajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza. 26. Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi tukufu. 27. Akasema (Suleiman): Tutatazama umesema kweli au wewe ni miongoni mwa waongo. 28. Nenda na barua yangu hii na uwafikishie, kisha waache na utazame watarejesha nini. 29. (Malkia) akasema: Enyi wahishimiwa! Hakika nimeletewa barua tukufu. 30. Imetoka kwa Sulaiman nayo ni: Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. 31. Msinifanyie jeuri, na fikeni kwangu nanyi mmekwisha kuwa wenye kusalimu amri. 32. Akasema: Enyi wahishimiwa! Nipeni shauri katika jambo langu hili, kwani mimi sikati shauri yoyote mpaka mhudhurie. 33. Wakasema: Sisi ni wenye nguvu na wakali kwa vita; na amri iko kwako, basi tazama ni nini unaamrisha. 34. Akasema: Hakika wafalme wanapo uingia mji wanauharibu, na wanawafanya wale watukufu wake kuwa wanyonge. Na hivyo ndivyo watendavyo. 35. Lakini mimi nitawapelekea zawadi, nami nitangoja watakayo rudi nayo wajumbe. 36. Basi alipo fika (mjumbe) kwa Suleiman, alisema (Suleiman): Hivyo ndio nyinyi mnanisaidia kwa mali? Aliyo nipa Mwenyezi Mungu ni bora zaidi kuliko aliyokupeni nyinyi. Lakini nyinyi mnafurahia hii zawadi yenu. 37. Rejea kwao! Kwa yakini sisi tutawajia kwa majeshi wasio yaweza kuyakabili. Na hakika tutawatoa humo na hali wao wamekuwa madhalili na wanyonge. 38. Akasema(Suleiman): Enyi waheshimiwa! Ni nani kati yenu atakaye niletea kiti chake cha enzi kabla hawajanijia hali ya kuwa wamekwisha salimu amri. 39. Akasema: Afriti, katika majini: Mimi nitakuletea kabla hujainuka pahala pako hapo. Na mimi kwa hakika nina nguvu na muaminifu. 40. Akasema mwenye ilimu ya Kitabu: Mimi nitakuletea kabla ya kupepesa jicho lako. Basi alipo kiona kimewekwa mbele yake, akasema: Haya ni katika fadhila zake Mola wangu Mlezi, ili anijaribu nitashukuru au nitakufuru. Na mwenye kushukuru, kwa hakika, anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake; na anaye kufuru, kwa hakika Mola wangu Mlezi ni Mkwasi na Karimu. 41. Akasema (Suleiman): Mgeuzieni kiti chake cha enzi hiki, tuone ataongoka, au atakuwa miongoni mwa wasioongoka. 42. Basi (Malkia) alipo fika akaambiwa: Je! Kiti chako cha enzi ni kama hiki? Akasema: Kama kwamba ndicho hichi. (Sulaiman na watu wake wakasema): Na sisi tumepewa ilimu kabla yake (Malkia), na tukawa Waislamu.))

Katika aya hizi tunajifunza mengine zikiwemo sifa za kiongozi na mambo ya kuyachunguza wakati wanasiasa wa wanaponadi sera zao ili tufanye uchaguzi wa busara na wenye maslahi. Kiufupi tunajifunza kama ifuatavyo:-

Sifa za Kiongozi mzuri:-

- Mwenye elimu, hekma na busara.

- Mwenye kumshukuru Allah na kuwathamini wenzake na wote anaowangoza.
- Alieandaliwa vyema kiuongozi ili aweze kuendeleza mazuri yalikapofikia. Aidha mwnye uwezo wa kuandaa viongozi watakaoendeleza atakapofikia
- Alie muadilifu na mwenye kuusimamia uadilifu na haki.
- Mwenye uwezo wa kutafuta, kupanga na kudhibiti rasilimali na nyenzo kwa nidhamu na uwezo wa hali ya juu.
- Uwezo wa kuvisikia vilio na kero za watu wa chini na uthubutu wa kuviitikia kwa haraka.
- Kutokuwa na kiburi kwa kukiri kutokamilika kwake hivyo kuwa tayari kukosolewa, kushauriwa na kuelekezwa.
- Awe ni mwenye kuthamini na kukiri juhudi na fadhila za waliomtangulia.
- Mwenye uwezo wa kufuatilia watendaji wa kada tofauti na uthubutu wa kuwawajibisha kwa mujibu wa utendaji wao.
- Msamehevu na mwenye kuchunga hali, dharura na mazingira yanavyokwenda.
- Mwenye kuhakiki taarifa anazopelekewa nakuzifanyia kazi.
- Mwenye dira, mikakati hai na anaejiamini katika kutoa maamuzi.
- Alietayari kupambana na rushwa katika hali zake zote.

Aidha tunafaidika kuwa mpiga kura anapaswa:-

- Kumuweka Allah mbele katika uchaguzi wake na kuchunga maslahi ya watu hivyo kutokubali kutumiliwa kwa lililo kinyume na amri za Allah.
- Kupima maneno na sera kabla ya kutoa maamuzi.
- Kuwa muaminifu.
- Kutambua kuwa Allah anamuuona na anayajua yaliyo moyoni mwake na atamuuliza kuhusu uamuzi aliochukua.

HITIMISHO

Ni jambo lisilo na shaka kuwa jamii ya Wazanzibari imejengwa kwa msingi madhubuti kabisa wa kiutamaduni. Msingi huo ndio uliowapa heshima na utukufu na kuweza kutajwa kwa sifa njema katika pande zote za Afrika na ulimwenguni kwa ujumla. Haya yanathibitishwa na kauli mashuhuri isemayo *" when the flute was played on Zanzibar, people danced along the lakes in the interior of Africa".*

Utamaduni huo wa kiislamu ndio unaowapatia watu nguvu na utukufu kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu ***((Allah amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya amali njema kuwa atawatawalisha katika ardhi kama alivyowatawalisha wale waliokuwa kabla yao na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hapo basi hao ndio wavunjao amri zetu)) {An Nur: 55***

Ni vyema kwetu kuhamasishana na kuhimizana kushiriki katika kuulinda utamaduni huo kwa kusikiliza sera za wanaoomba ridhaa ya kuwa viongozi na kutoa maamuzi ya busara katika kuchagua kwetu. Tuhimizaneni kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu na tumuombe Allah atubariki na kutuletea neema kutoka mbinguni na ardhini. Wabillah tawfiq.